

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**02 JUNI, 2016**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA TANO – 02 JUNI, 2016

### I. MASWALI:

#### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

#### 284. MHESHIMIWA AIDA JOSEPH KHENANI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kumekuwa na hali ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na Mgambo na Askari Polisi wanapotekeleza maagizo ya Serikali dhidi ya wafanyabiashara wadogo wadogo hususan mama lishe, bodaboda pamoja na machinga:-

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya hali hiyo.

#### 285. MHESHIMIWA STANLAUS HAROON NYONGO (MASWA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mhe. Rais Mstaafu Dkt. J.M. Kikwete aliahidi kujenga barabara za Mji wa Maswa zenye urefu wa km 3 ndani ya Halmashauri ya Mji mdogo wa Maswa:-

Je, ni lini barabara hizo zitaanza kujengwa.

## **WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

### **286. MHESHIMIWA ABDALLAH HAMIS ULEGA (MKURANGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itawasaidia Wananchi wa Wilaya ya Mkuranga kwa kuwaunganisha kwa barabara ya moja kwa moja kutoka Mkuranga – Kisarawe – Kibaha bila ya kupitia Mkoa wa Dar es Salaam.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **287. MHESHIMIWA MUSA RASHID NTIMIZI (IGALULA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Wilaya ya Uyui ni Wilaya Mpya ambayo makao yake Makuu yako Isikizya na Jeshi la Polisi tayari limehamia yaliko Makao Makuu ya Wilaya lakini mazingira ya hapo kwa Askari Polisi ni magumu sana kwa sababu hakuna maji, hakuna nyumba za kuishi Askari hao, ambao kwa sasa wanaishi kwenye nyumba za kupanga au kwenye mabanda ya mabati yaliyojengwa karibu na kituo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha mazingira hayo kwa Askari wetu ili wafanye kazi katika mazingira bora zaidi.



**288. MHESHIMIWA MWANTUMU DAU HAJI  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Askari wa usalama barabarani ndio wenye dhamana ya kuhakikisha usalama kwa watumiaji wa barabara, lakini kwa sasa askari hao wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya rushwa na ukosefu wa maadili:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Askari wa Usalama barabarani wanakuwa waadilifu na hawajihusishi na vitendo vya rushwa.

**289. MHESHIMIWA ALLY KEISSY MOHAMED  
(NKASI KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Vituo vya Polisi vya Kabwe na Kirando vimechakaa sana na hata Polisi hawana nyumba za kuishi:-

Je, ni lini Serikali itajenga au kukarabati vituo hivyo na kuwajengea Polisi nyumba za kuishi.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

**290. MHESHIMIWA MUHAMMED AMOUR MUHAMMED (BUMBWINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:- Kwa muda mrefu kumekuwepo na tatizo la wanafunzi wanaoingia vyo vikuu kukosa mikopo; na elimu ya juu ni suala la Muungano:-

Je, Serikali ya Muungano inaipatia SMZ kiasi gani cha fedha kwa mwaka kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi hao.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**291. MHESHIMIWA VEDASTO EDGAR NGOMBALE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Napongeza jitihada za Serikali kwa kuanzisha mradi wa maji katika kijiji cha Mingumbi, ambao utakapokamilika utawezesha Wananchi katika Vijiji vya Mbingumbi, Kilelima, Naipuli, Njianne, Tingi, Mtandango na Miteja kuondokana na tatizo la maji. Hata hivyo tatizo la maji bado ni kero kubwa katika maeneo mengi ya Jimbo la Kilwa Kaskazini na Wilaya ya Kilwa kwa ujumla:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha mradi mkubwa wa maji kutoka katika Mto Rufiji ambao upo jirani na Wilaya ya Kilwa kwa madhumuni ya kumaliza kabisa kero sugu ya maji inayowakabili Wananchi wa Wilaya ya Kilwa.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**292. MHESHIMIWA DOTO MASHAKA BITEKO (BUKOMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Maafisa wa Idara ya Wanyamapori walivamia wananchi wa Kitongoji cha Idosero kilichosajiliwa kwa GN na kuchoma nyumba 40 za wananchi na kuharibu mazao yao:-

- (a) Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Idosero kwa hasara kubwa waliyoipata;
- (b) Wananchi wa Wilaya ya Bukombe wanapakana na Mapori ya akiba ya Kigosi, Muyowosi na Wananchi wafugao Nyuki kwenye mapori haya wanapata usumbufu mkubwa wa kufuata vibali vya kuingia porini Wilayani Kahama, Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga Ofisi wa ndogo ya Maliasili Bukombe.

**DODOMA  
02 JUNI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**